

HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWA

SEHEMU YA MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA WATAALAMU (CMT) KILICHOFAANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE 25/03/2022

WALIOHUDHURIA:

1.	Ndg	James C Chitumbi	- Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)	- Mwenyekiti
2.	"	Juvenary P. Mpanga	- Kaimu Afisa Utumishi na Utawala (W)	- Katibu
3.	"	Isihaka Mbegha	- Afisa Uchaguzi na Utawala Bora (W)	
4.	"	Douglas P.Mwela	- Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (W)	
5.	"	Mabula K.Isambula	- Afisa Ardhi na Maliasili (W)	
6.	"	Deonis Sui	- Mweka Hazina (W)	
7.	Dk	Emmanuel Kassian	- Kaimu Afisa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (W)	
8.	Ndg	Joseph Kalolo	- Kaimu Afisa TEHAMA na Uhusiano (W)	
9.	"	Aloyce R. Msigala	- Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo	
10.	"	Joseph Makyao	- Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)	
11.	"	Bahati E. Kikoti	- Mwanasheria (W)	
12.	"	Erick T. Sezary	- Afisa Usafirishaji (W)	
13.	"	John S.Malibichi	- Kaimu Afisa Elimu Msingi (W)	
14.	"	Innocent Msofu	- Mkaguzi wa Ndani (W)	
15.	"	Alexander M. Chang'a	- Kaimu Afisa Ugavi na Ununuzi (W)	
16.	Dk	Libamba Sobo	- Mganga Mkuu (W)	
17.	Ndg	Ashraf Bigge	- Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)	
18.	"	Casmir Combo	- Kwa Niaba ya Katibu Tawala (W)	
19.	"	Goodluck J. Kalambani	- Kaimu Afisa Ufugaji Nyuki (W)	
20.	"	Alice Nkwera	- Kaimu Afisa Elimu Sekondari(W)	
21.	"	Peter Ngusa	- Afisa Mipango Takwimu na Ufuatiliaji (W)	

SEKRETARIET:

1. Masoud S. Mpota

AJENDA NA.KDC/FUM/01/07/2021/2022 - KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwakutanisha Wajumbe katika Kikao cha dharula cha kujadili taarifa ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa fedha za TCRC (UVIKO 19). Alifungua kikao saa 03: 20 Asubuhi.

AJENDA NA.KDC/FUM/02/03/2021/2022 -KURIDHIA AJENDA

Wajumbe waliridhia ajenda zifuatazo:

1. Kufungua kikao

2. Kuridhia ajenda
3. Taarifa ya kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vya Madarasa 42 vinavyotokana na fedha ya TCRC (UVIKO 19).
4. Kufunga kikao.

AJENDA NA.KDC/FUM/03/03/2021/2022 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA AJENDA

Ajenda zilisomwa na kuridhiwa na wajumbe wa kikao na mwenyekiti kuendelea na kikao kwa ajenda zilizofuata.

AJENDA NA.KDC/FUM/04/03/2021/2022 - TAARIFA YA KUKAMILIKA KWA UJENZI WA VYUMBA 42 VINAVYOTOKANA NA FEDHA YA TCRC (UVIKO)

Afisa Mipango Takwimu na Ufuatiliaji (W) Kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vya Madarasa 42 ambapo kati ya vyumba hivyo 37 ni Madarasa ya shule za sekondari na Matano (5) ni shule shikizi ya Mzenga B kwa kuelezea kiasi ambacho shule imepata na ujenzi ulipofikia kama inavyoonekana katika jedwali,

NA	JINA LA SHULE	IDADI YA MADARASA	KIASI CHA FEDHA KILICHOTUMIKA	HATUA YA UJENZI ILIPOFIKIWA
1	CHOLE	2	40,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
2	KIBUTA	5	100,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
3.	MAKURUNGE	1	20,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
4	GWATA	3	60,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
5	GONGONI	2	40,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
6	MANEROMANGO	3	60,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
7	MFURU	3	60,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
8	MASAKI	3	60,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
9	JANGUO	2	40,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
10	MSIMBU	5	100,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
11	MZENGA	3	60,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
12	VIKUMBURU	2	40,000,000.00	Ujenzi umekamilika

NA	JINA LA SHULE	IDADI YA MADARASA	KIASI CHA FEDHA KILICHOTUMIKA	HATUA YA UJENZI ILIPOFIKIWA
				madarasa yanatumika
13	MLOGANZILA	3	60,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
14	MZENGA B (SHIKIZI)	5	100,000,000.00	Ujenzi umekamilika madarasa yanatumika
JUMLA			840,000,000.00	

Ambapo aliendelea kueleza kuwa ujenzi umekamilika katika shule zote 14 (Shule za Sekondari 13 na shule ya Msingi 1 (Shikizi)) na madarasa yanatumika.

Aidha baada ya uwasilishaji kufanyika Wajumbe walitaka kupata maelezo kutoka kwa Muhandisi kuhusiana na ubora wa Madarasa kulingana na miongozo na kiasi cha fedha kilichotumika.

Muhandisi ujenzi (W) alieleza kuwa Madarasa yote yamejengwa kwa kufuata vigezo na taratibu zilizowekwa ambazo kabla ya kuaza ujenzi walielezwa katika kikao kilichofanyika tarehe 29/10/2021 na walipwea maelekezo kwa maandishi, hivyo Mafundi wamejenga kwa kufuata maelekezo hayo kwa madarasa yote na Madarasa yote ni bora na yamekamilika kama ambavyo ilikusudiwa.

Hitimisho: Taarifa ilipitishwa.

AJENDA NA.KDC/FUM/04/03/2021/2022 - KUFUNGA KIKAO

Kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao, aidha alisisitiza suala la umoja na ushirikiano katika majukumu ya kazi.

Alifunga Kikao saa 7:00 Mchana.

MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA HAPA KISARAWE TAREHE 25/ 03/ 2022 NA:-

JINA: Juvenary P. Mpanga

JINA: JAMES C. CHITUMBI

SAINI

SAINI

KATIBU

MWENYEKITI